## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI AGOSTI, 2026 NA MWELEKEO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2026.

**Dondoo za tathmini ya Agosti, 2026 na mwelekeo wa Septemba, 2026:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Agosti, 2026 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa hususan hali ya joto kwa mwezi Septemba, 2026 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2026 maeneo mengi nchini yaliendelea kupata vipindi vya baridi ya wastani hadi baridi kali, hususan nyakati za usiku na asubuhi.
ii. Vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Agosti 2026, hususan ukanda wa pwani, kanda ya kati pamoja na maziwa makuu. Aidha, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani, ukanda wa ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.
iii. Katika kipindi cha mwezi Septemba 2026 vipindi vya baridi ya vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, Ziwa Victoria, na nyanda za juu kaskazini mashariki. Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo.

## 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI AGOSTI, 2026.


Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2026 hali ya ukavu ilijitokeza katika maeneo mengi ya nchi iliyoambatana na hali ya baridi ya wastani hadi baridi kali kwa baadhi ya maeneo, hususan nyakati za usiku na asubuhi. Kiwango cha chini kabisa cha joto cha nyuzi joto 5.0 °C kiliripotiwa katika kituo cha Uyole (mkoa wa Mbeya), ikifuatiwa na nyuzi joto 5.5°C katika kituo cha Igeri mnamo tarehe 2 Agosti 2026.

Vipindi vya upepo mkali unaofikia kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ukanda wa pwani, maziwa makuu na kanda ya kati. Aidha, vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 53.4 kilirekodiwa katika kituo cha hali ya hewa Zanzibar mnamo tarehe 21 Agosti, 2026.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 03/2026*




**Kielelezo 1**: Viwango vya joto la chini kwa vituo vya Uyole na Igeri katika mwezi Agosti, 2026.

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI SEPTEMBA, 2026

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Joto la Bahari katika eneo la tropiki ya kati ya Bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, ikiashiria kuanza kuimarika kwa hali ya El Niño. Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi, karibu na Pwani ya Afrika mashariki, linatarajiwa kuwa la juu ya wastani, wakati eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la bahari la chini kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuongeza upepo wenye unyevu kuvuma kuelekea ukanda wa pwani ya nchi yetu na mikoa ya jirani. Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa Bahari ya Atlantiki, karibu na pwani ya Angola linatarajiwa kuwa la chini kidogo ya wastani.

Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (kusini mwa kisiwa cha Madagascar) linatarajiwa kuendelea kua la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudhoofisha mgandamizo mkubwa wa hewa wa Mascarene na hivyo kupunguza kasi ya upepo wenye baridi unaovuma kutoka kusini kuelekea katika maeneo ya nchi yetu.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2026

Kipindi cha mwezi Septemba 2026, viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kadri Msimu wa Kipupwe unavyoendelea. Hali ya baridi zaidi (chini ya nyuzi joto 10) inatarajiwa kujitokeza katika maeneo ya nyanda za juu Kusini magharibi pamoja na kusini mwa nchi hususan nyakati za usiku na asubuhi.

Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya ukanda wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo yenye miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine, vipindi vifupi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ya ukanda wa pwani na maziwa makuu na kati mwa nchi.  Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 26 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani. Aidha, katika maeneo ya nchi kavu, viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C na 22 °C. Vipindi vifupi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 13 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 13 °C. Kwa ujumla hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi pamoja na vipindi vichache vya mvua, hususan katika maeneo ya miinuko.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Aidha, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 14 °C. Kwa upande mwingine, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16°C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Kwa ujumla, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi pamoja na vipindi vichache vya mvua.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya baridi kali inatarajiwa katika maeneo ya miinuko ambapo joto la chini linatarajiwa kuwa chini ya nyuzi joto 8 °C ikiwemo baadhi ya maeneo ya mkoa wa Njombe. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea kujitokeza katika maeneo mengi.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10°C hadi 18°C katika maeneo mengi. Aidha, maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 °C. Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 03/2026*

**2.3 MATARAJIO KWA MWEZI OKTOBA, 2026**

Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2026 mvua za Vuli zinatarajiwa kuanza katika maeneo yapatayo misimu miwili ya mvua. Aidha, ongezeko kidogo la joto linatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi pamoja na vipindi vifupi vya upepo mkali katika maeneo machache,

**2.4 USHAURI**

Tahadhari za kiafya zichukuliwe ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa yanayoweza kusababishwa na baridi, vumbi na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi katika kipindi hiki, maji na malisho yanapaswa kutumika kwa uangalifu ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Septemba, 2026 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz